

## **Mwongozo wa Mpango wa Kutia Umeme katika Magari Yako**

### **Muhtasari wa Mpango**

Shirika la Uchukuzi lina furaha kutangaza uzinduzi wa Mpango wa Kutia Umeme katika Magari Yako ili kuhimiza utiaji umeme kwenye magari na kupunguza athari za tabianchi kutokana na magari ya kibiashara, ya manispaa, na ya mashirika yasiyokuwa ya kibiashara. Mpango huu wa kutia motisha utawasaidia wamiliki wa biashara kufadhili ubadilishaji wa injini zinazotumia mafuta (ICE) na kutumia magari safi zaidi yanayotumia umeme (EVs) au kuepuka kuongeza magari yanayotumia mafuta kwenye kundi lao la magari. Kwa pamoja na motisha nyingine za shirikisho, jimbo, na matumizi ya umeme, wamiliki wa makundi ya magari wanaostahiki huenda wakapata fursa ya kuokoa maelfu ya dola kupitia chaguo la usafiri safi.

### **Ustahiki**

Mpango huu wa ruzuku ya \$500,000 unapatikana kwa wamiliki wote wa magari ya kibiashara, manispaa na mashirika yasiyo ya kibiashara waliosajiliwa katika Vermont kwa misingi ya jimbo lote, ya huduma kwanza kwa anayejisajili kwanza.

Utoaji utafanyika katika njia ya ulipaji wa hadi \$2,500 kwa kila gari linalotumia mafuta ambalo linabadilishwa au kutotumiwa kukiwa na kiwango cha juu zaidi cha motisha 20 kwa kila kundi la magari katika kipindi chote cha mpango huu. Mashirika yasiyokuwa ya kibiashara ya huduma za usafiri yanayowapa Wakazi wa Vermont mbinu mbadala za uchukuzi wanastahiki hadi motisha 5 za kiasi kilichoimarishwa cha \$5,000 kama nyongeza kwa hadi motisha 15 kwa kiwango cha kawaida cha \$2,500.

Ufadhili huu utatumiwa katika ununuzi au ukodishaji wa magari yanayotumia umeme (PEVs) au chaguzi nyingine za makundi ya magari ikiwemo baiskeli za umeme, baiskeli za umeme za kubebea mizigo, baiskeli za umeme zinazobadilika, pikipiki za umeme, au magari ya umeme ya kutumika katika theluji.

Wanaoomba lazima waonyeshe kwamba magari yatakayofadhiliwa yatachangia kupunguza uzalishaji wa gesi chafu.

Magari yote yatakayonunuliwa au kukodishwa kupitia mpango huu lazima yamilikiwe na mwombaji kwa muda usiopungua miezi ishirini na nne (24) na juhudi za haja lazima zifanywe kuyauza magari haya kwa wauza magari ambao wanashiriki katika Mpango wa MileageSmart, ambao ni Mpango wa Vermont wa motisha kwa msingi wa ustahiki kimapato kwa magari yaliyotumika.

## Mchakato wa Kutuma Maombi

Ili kuomba kushiriki katika Mpango wa Kutia Umeme Magari Yako, wamiliki wa makundi ya magari lazima wajaze fomu ya maombi mtandaoni. Maombi yatakaguliwa na kamati inayojumuisha wafanyakazi wa Shirika la Uchukuzi. Mawasiliano yatafanywa na waliotuma maombi kupitia simu za uchunguzi ili kuthibitisha ustahiki na kuweza kutoa hati za kuthibitisha. Waombaji wote wanahimiza kupitia kwa makini Notisi ya Fursa ya Ufadhili (NOFO), Miongozo ya Mpango, na nyenzo za ziada zilizopo kutoa msaada na kufadhili juhudi za kutia umeme katika magari zinazopatikana kupitia [Tovuti ya Shirika la Uchukuzi](#).

*Iwapo wewe si **mnenaji wa Kiingereza** na unahitaji msaada wa tafsiri, tafadhali wasiliana na wafanyakazi wa Shirika la Uchukuzi kwa kutuma barua pepe kwa [AOT.climate@vermont.gov](mailto:AOT.climate@vermont.gov) ili uunganishwe na huduma za tafsiri na ukalimani zilizolipiwa na Jimbo. Tafadhali tupatie jina lako, nambari ya simu, na anwani ya barua pepe ili tuweze kuwasiliana nawe tukiwa na mtafsiri wakati wa saa za kazi, saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni.*